pale yameingiliwa na kuathiriwa na tamaduni za kigeni, kwa mfano Kiarabu na Kizungu. Na hiki ndicho chanzo kikuu cha kuhitilafiana wahusika wake katika kila mchezo.

## PAMBO

### *Utangulizi*

Mchezo huu wa kuigiza ni wa nne katika mlolongo wa vitabu vya Mama P. O. Mlama (hapo awali akijulikana kwa jina la P. Muhando). Vitabu vyake vingine ambavyo vimekitangulia hiki ni *Heshima Yangu* (EAPH), *Tambueni Haki Zetu* (TPH) na *Hatia* (EAPH).

### *Muundo na Mtindo*

Muundo wa mchezo huu ni tofauti na ule wa *Heshima Yangu, Hatia* na *Tambueni Haki Zetu.* Katika michezo yake mingine, Mama Mlama alitumia muundo wa kawaida. Muundo uliozoeleka na waandishi pia na watazamaji wengi.

*Pambo* ni mchezo wa hali ya juu kimuundo. Hapana shaka yo yote kwamba Mama Mlama kama Ebrahim Hussein, ameathiriwa sana na Bretcht, mwandishi hodari na wa pekee wa michezo ya kuigiza ya kimashariki. Kwa mtu aliyesoma Mashetani (OUP) hatasita kusema kuwa Mama Mlama kaathiriwa na Ebrahim Hussein katika uandishi wake. Jambo hili liwe ni kweli ama sivyo, si jambo la msingi bali la maana zaidi ni kufahamu tu kwamba waandishi hawa wawili wamejitokeza kuwa mafundi na mabingwa wa kuandika michezo.

*Mashetani* kimeandikwa kishetani shetani. Kusomeka kwake na kufahamika kwake pia ni kwa kishetanishetani. Ama msomaji ajifanye shetani au ajihisi kuwa na yeye ni mmojawapo.

Pambo kimeandikwa kiwendawazimu wendawazimu bali hali ya mchezo imemlazimisha kuwa hivyo wakati akiuandika mchezo huu. Haya ni mashtaka ya kawaida juu ya waandishi. Aandikaye juu ya upelelezi sharti asemwe kuwa naye yu mpelelezi. Kadhalika juu ya ujamaa ama ubepari, sheria, ndoa, n.k. Na sisi wasomaji twapaswa kukubali kuwa vichaa ndipo tuone raha ya kusoma mchezo huu na kuufahamu. Si kichaa cha kutumia nguvu na kufanya madhara bali zaidi ni kichaa cha mawazo.

### *Mandhari*

Mchezo unaanzia nyumbani mwa Pambo. Kakaa akitazama mchezo wa cheti na joho—mchezo wa Pambo la kisomo. Nasi tunamtazama yeye akitazama mchezo. Tunapewa nafasi ya kuutafakari huo mchezo. Kisha tunaona mchezo mwingine. Nao ni wa Maua. Kwanza tunamwona Maua kwa macho ya moyoni akiwa kituoni akisubiri mabasi. Kwa wakazi wa Dar es Salaam, hali hiyo ndiyo kawaida ya maisha (1970's). Mtu anaweza kukaa saa

tatu au nne kituoni. Kwa hiyo huu ni mchezo wa kweli ambao mandhari yake yako katika hisia za ujuzi wa mambo. Pili tunamwona Maua kwenye kichaa. Anamsemesha mtu asiyemjibu lo lote. Badala yake Pambo anakisemesha cheti na joho. Anacheka na kuimba. Kwa hiyo Maua anaonekana akitazama mchezo wa Pambo na rafiki zake cheti na joho na kumsikiliza anavyosema nao, kuimba na kucheza. Baadaye wanajiunga wakina Pesa na Raha. Blaza anapowajia akina Pambo anashangaa. Anajaribu kumsemesha Pambo anashindwa. Kisha kunatokea ugomvi baina ya Maua na Wema—Onyesho la kwanza linamalizika kwa ushindani wa matusi na kushikiana viti baina ya Maua na Wema. Sisi wasomaji ambao labda ndio watazamaji tunaona mengi.

Onyesho la Pili linatupeleka porini ambako tunawakuta Pambo, Pesa na Raha, wamechoka, wamedhoofika na kuchafuka sana. Ili mchezo ukidhi haja iliyokusudiwa, mandhari ya onyesho hili lazima yawe porini. Labda pori la hisia au la kiwendawazimu, lakini hasa ni pori, pori ndilo lenye kuweza kukidhi kiu hichi. Wakati tukitazama mchezo wa akina Pambo, kina Baba Pambo nao wanaingia; wanatufika porini. Wao wamekuja kuwatafuta watoto wao ili wawarudishe nyumbani. Onyesho hili linakwisha na wazo la kutafuta mganga.

Onyesho la Tatu linaturudisha tena porini, tunamtazama mganga akiwaongoza akina Baba Pambo wakiwataka watoto wao. Wakati wa msako huu, kunatokea kimchezo ndani ya mchezo (uk. wa 35). Katika kimchezo hiki tunadhihirishiwa zaidi na kimchezo kingine (uk. wa 36) juu ya matumizi ya raha ya pesa. Baada ya hapo tunatazama mchezo wa kikundi cha Mganga kinavyokitaka kikundi cha Pambo kwa maarifa ya kiwendawazimu.

Mchezo unamalizika kwa matumaini makubwa ambayo bado yanasisitizwa na sauti kwamba kichaa tulichonacho siyo kichaa cha kutumia nguvu na kufanya madhara bali zaidi kichaa cha mawazo.

Mtindo wa mwandishi wa kutiatia vijimchezo umeusaidia sana muundo wa mchezo huu kuonekana na kudhihirika na hasa kupunguza hali ya kukata tamaa au uchovu wa kuusoma mchezo wenyewe. Na hasa mtindo wa kutushirikisha wasomaji (watazamaji) katika kuwatafuta na kuwatazama kila linalowapata akina Pambo.

Hata hivyo, baadhi ya wasomaji hawatakuwa wamekosea sana iwapo watausema mchezo huu kuwa ni wa kitoto. Kitoto kwa maana ya kutoifanyia haki mchezo wenyewe. Kwamba mwandishi amekusudia kusema neno kubwa sana lakini kalisema kitoto. Ama kalisema kiwendawazimu. Na mtu asipokubali kuwa mwendawazimu basi mchezo huu wote utakuwa hauna thamani sawa na vile alivyo ama achukuliwavyo mwendawazimu ye yote. Na wengine watasema huu ni ufundi wa mwandishi wa kusema maneno makubwa sana kwa kutumia vichaa. Basi ikiwa kichaa aweza kuliwakilisha jambo lenye uzito kiasi hiki, tulio wazima ama tujidhaniao kuwa tu wazima, tutalichukuliaje? Tutalisema vipi? Tutalijadili vipi? Haya ni baadhi ya mambo muhimu yanayohitaji majadiliano makali na mazito. Kazi hii twaiachia darasa—mwalimu na wanafunzi wake.

***Wahusika***

***Pambo:*** Mhusika huyu ni kama wahusika wawili kwa mmoja. Ni mtu, na pia ni pambo. Kwa kuwa cheti cha shahada pamoja na joho la sherehe ya kupatia shahada kwa Pambo vimekuwa pambo, nasi twamchukua Pambo mtu kumfanya pambo. Kwa sababu hii wazo la kukiona kisomo au elimu kuwa pambo linadhihirika. Na kutokana na hali hii ya kuifanya elimu kuwa pambo pamoja na wasomi wenyewe kuwa na pambo, hali ya maisha katika nchi zetu imekuwa pambo na kila mtu ni pambo. Hali hii ndiyo isababishayo watu kuwa na mawazo mengi mazito ambayo hayakuhusu hasa matatizo ya jamii kama jamii bali yahusu matatizo yao binafsi. Mwisho wake ni kuwa na akina Pambo kila pembe ya dunia.

Pambo mtu ndiye mhusika mkuu wa mchezo huu. Ndiye yeye anayeiwakilisha na kuidhihirisha dhamira na ujumbe wa mchezo huu. Maneno anayosema yanatusaidia kujua sababu za kupatwa kwake na kichaa cha mawazo. Anawakilisha migogoro na migongano inayotokea baina ya wasomi na jamii zao. Historia imetuzoeza kuheshimu kisomo na elimu ya juu. Kwamba mtu mwenye kisomo cha juu hupewa madaraka makubwa na kwa sababu hiyo hutarajiwa kuwa na mamlaka na wajibu mkubwa kazini na maishani. Na kuna wengi wanaoamini hivyo na kwamba hii ndiyo hali ya kweli iliyoko ulimwenguni hivi leo.

Hata hivyo tusisahau kuwa wasomi ni binadamu na kila mwanadamu ana sifa ama ila zake. Kuna baadhi ya wasomi ambao waliamini baadhi bado wanaamini kwamba mradi Mwingereza (Mtawala) hayuko wao watachukua nafasi hizo. Ingekuwa kheri sana kama wasomi hao wangerithi sifa ya ufanisi wa kazi namna ya usemaji. Huu ni mgogoro mmojawapo ambao Pambo anakutana nao. Kwamba kuwa kwake Mkurugenzi Meneja amekuwa mtu mwenye ujuzi wote. Kwa upande ni kweli kwamba yeye ni mtaalam, hivyo ni muwakilishi wa kundi lake. Lakini pia si mtaalam wa kujua yote kwani hali hii ndiyo impayo kiburi mpaka anashindwa na maisha. Ofisi yake kubwa iliyojazwa mazulia na simu nyingi, meza na viti vya kila namna, kama kweli, anayo, ndiyo imzidishayo kiburi na fakhari ya kichaa; maana tangu kazi anayofanya na ofisi anayofanyia, si lo lote si cho chote bali ni pambo, pambo, pambo.

Pambo anasema ana gari ambayo haipandiki. Ana nyumba ya vyumba sita vya kulala Pambo na vitatu vya wageni. Ana vyombo ambavyo hata Ulaya hakuna. Kiu chake kikubwa katika maisha ni wasichana na anasema anao tele tele. Labda ndoto ya vyombo ni ndoto nzuri kwa kuwa inazihimiza nchi changa kujitengenezea vyombo vyao ambavyo vitakuwa bora zaidi ya hivyo vitokavyo Ulaya. Vinginevyo ni fakhari ya kiwendawazimu ambayo haina maana hata kidogo. Fakhari ambayo inamtia kichaa Pambo. Lakini mwishoni Pambo anaonyesha matumaini. Anajiuliza maswali ya msingi; kwamba yeye ni pambo gani, pambo la aina gani na anapamba nini.

***Maua***

Ni msichana wa umri wa miaka 18—20. Rafiki yake Pambo. Yeye

anawakilisha mawazo ya wasichana wenzake wenye fikra kama zake. Je, anatuambia nini. Kwamba mjini kuna taabu ya mabasi, amengoja basi kwa saa tatu nzima asilipate. Miguu na mwili mzima unamwuma. Kwake; labda kuwa na gari ni jambo la starehe. Lakini kama angekuwa anakwenda kazini; baada ya kusubiri mabasi kwa saa tatu na zaidi, angeweza kuifanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa? Au tukubali tu kuwa gari ni pambo kwa watu wote?

Pambo ni Mkurugenzi Meneja. Bila shaka anayo gari, kama si yake binafsi, ya kazini. Maua anamlaumu kwa kutonunua gari; atuambia kuwa kazubaa mpaka Serikali imekataza kununua magari ya binafsi. Maua anamsuta Pambo kwa kushindwa kununua gari, hata la sekenihendi. Pia kwa kutokuwa na pesa za kwenda sinema ya God Father. Anamwamuru atoke akatafute pesa. Je, mshahara mkubwa wa Pambo u wapi? Ndani mwake hamna bia wala soda ingawa labda amewahi kukopa friji.

Baada ya kusema maneno yote hayo, Maua anajihisi ubwege kwa kuwa Pambo hana analomjibu. Kwa hiyo naye ana kichaa kama alichonacho Pambo kwa kutamani vitu asivyo na uwezo navyo. Hata hivyo, yeye ni mmoja kati ya wengi wenye kumdhuru Pambo. Ni mwakilishi wa wasichana wa kimiji ambao aghalabu kazi yao kubwa ni kujipodoza na kusubiri wanaume wa kuwapeleka huku na kule na kuwasababishia madeni mengi yasiyo na sababu. Labda ni kwa sababu ya ujinga wa kiume kama si hila za kike za kuwanyonya wanaume. Tatizo lote hili latokana na mapambo ya kilimwengu.

***Raha na Pesa***

Wavulana wa umri wa miaka 10—15. Wamemzoea Pambo. Labda wamemzoea Pambo kwa sababu wao wenyewe ni pambo la Pambo. Raha ndicho kiini cha mgogoro na tatizo la Pambo. Ndicho kitu cha msingi katika maisha yake. Ingawa kila binadamu anapenda raha lakini raha ya Pambo si raha bali raha ya kumpatisha dhiki. Raha ya kutaka kuwa na wasichana wote wa ulimwenguni. Raha ya fakhari isiyo na maana. Mradi ni haraka kwake na ni kirihi kwa wengine. Pesa ni pesa. Ni maua. Mwenye pesa ndiye awaye na raha. Kwa hiyo vijana hawa wanapofuatana naye na kudai rekodi ya "The Jacksons" na baadaye kucheza *soul* wanawakilisha hali ya kweli ya maisha ya akina Pambo. Maisha ya vijana. Vijana wasio na mashiko. Vijana huru wasio na uhuru. Raha na Pesa ni marafiki wa ubongo wa Pambo. Kwake, maisha ni raha na pesa tu. Kwa kuwa Pambo ni kichaa, Raha na Pesa nao pia ni vichaa.

***Blaza***

Kijana wa umri wa miaka 26—30. Rafiki wa Pambo. Ndiye mtu anayewafuma akina Pambo wakiimba na kucheza. Anashindwa kuimudu hali anayowakuta nayo. Anaomba msaada. Ndiye mtu anayejaribu kuieleza hali aliyonayo Pambo:

> Sijui hasa. Labda tuseme basi ni kichaa.
> Lakini siyo kichaa cha kutumia nguvu kuleta
> madhara, bali zaidi kichaa cha mawazo. Unge-
> yasikia maneno aliyokuwa akiimba! (uk. wa 18).

Kisha anawahimiza akina Mama Doto kumtafuta Pambo. Wema anaachwa nyumbani na akina Blaza wanakwenda kuwatafuta akina Pambo.

Kwa machache yanayomhusu tunamwona kwamba kweli yu rafiki wa Pambo. Ana uchungu wa hali ya rafiki yake ingawa baadaye hatumwoni tena katika juhudi za kumtafuta.

***Wema*** ni msichana wa umri mkubwa zaidi kuliko wa Maua. Anaonekana kuwa rafiki wa kweli wa Pambo. Ana uchungu na Pambo na kwake Maua ni mchawi wa Pambo, mfilisi wa mali yake, mwizi, mnyang'anyi na kwamba mapenzi ya Maua ni ya pesa.

Labda umri mkubwa wa Wema na malezi bora ya wazazi wake ndiyo yampayo hali na hadhi aliyonayo. Mawazo yake ni mazuri na analaani vikali mwenendo mchafu wa akina Maua ambao mijini wanaitwa "dogi seksheni"—kikundi cha mbwa, watoto wa mbwa, mbwa mwitu. Matusi anayotukana na kupigana anakotaka ni kwa kujikinga lakini si kwa uchokozi na uhayawani wa Maua. Ama kama Pambo angekuwa mtu wa kutamani kuoa, labda Wema angekuwa mkewe kwani mapenzi yake yalilenga hilo.

Wema anaitwa, anaitika. Wanaachana na Maua ambaye mpaka mwisho wa onyesho hili la kwanza anaonekana yu mshenzi, mgomvi, mwizi, mnyang'anyi, mbwa mwitu, mradi si mtu kwa lo lote. Wema ana sifa ya kuweza kuigwa. Ingawa na yeye yumo katika jumla ya watu waliosababisha kichaa cha Pambo. Pia jina lake laweza kuwa sababu nyingine iliyompumbaza Pambo mpaka akatokwa na akili na kuwa kichaa kwani kama wasemavyo Waswahili "wema ujinga."

***Mama Doto***

Mama wa makamu; jirani wa Pambo. Ni mtu anayesikia na kuona mengi kuhusu Pambo na nyumba yake. Anaeleza waziwazi mawazo yake juu ya wasichana wa Pambo hasa Maua na wengine wa aina yake:

"Lakini kitu kimoja kinanishangaza. Nilimwona yule msichana wake, yule mwenye kuvaa mapekosi na manywele ya kubandika. Yule mwenye kujisiliba mawanja . . . ." (uk. wa 19).

> "Mimi nakwambia, yule msichana bila shaka kamtupia jini. Yule msichana yuko kishetani shetani. Kamloga Pambo. Simpendi yule msichana. Huwa sipendi hata apite nje ya nyumba yangu . . ." (uk. wa 19).

Haya ndiyo mawazo ya akina mama wa umri wa miaka 30—35. Ama wanaweza kusemwa ni watu wa zamani lakini kusemwa huko sharti kuambatane na sababu za maana. Maua si mtu. Labda ni kwa sababu ya pesa, lakini mbona wako wasichana wengi wa umri wake ambao hawana tabia hiyo ya kimbwa mwitu? Je, mabadiliko haya ya kuthamini pesa badala ya utu ni ya akina Maua tu? Je, wazazi wao wanaweza kuwa sababu ya mwenendo huo? Au jamii nzima inahusika? Hili ni suala zito na kubwa. Linahitaji kutazamwa

kwa undani mkubwa tukizingatia taratibu zetu za utamaduni ambazo kwa sasa zinaathiriwa sana na mfumo mpya wa uchumi. Kwa vyo vyote wazazi, walimu na jamii nzima kwa jumla tunahusika na ubovu huu ambao siku hadi siku unazidi kukua na kutuharibu. Kwa watu watakao uhuru usio uhuru, raha ya kiwendawazimu kama ya akina Pambo na wasiothamini mipaka ya utu wao wala heshima ya jamii zao, ila za akina Maua si ila bali ni maendeleo ya mabadiliko ya mfumo wa jamii. Mawazo haya hayajengi bali yanabomoa. Hata hivyo hili nalo ni suala la majadiliano baina ya walimu na wanafunzi na kati ya wanafunzi wenyewe kwa wenyewe.

Pamoja na hayo, Mama Doto anaonekana kuwa jirani mwema mwenye moyo wa huruma. Anashauri kuwatafuta akina Pambo. Mama Doto na Blaza ndio watu wa kwanza wanaoanza kuwatafuta akina Pambo.

Mwisho tunamwona na kumsikia akimrudia Wema ili wasaidiane kuwakamata akina Pambo. Mama Doto ni mwanamke mwenye moyo wa imani na ushujaa. Ni mama anayestahili sifa na pongezi. Nafasi aliyopewa na mwandishi ni ndogo lakini kama angemshirikisha, labda angeweza kushauri njia nzuri zaidi ya kuwaokoa akina Pambo.

*Baba Pambo*

Ni mtu mzima. Ni mzazi. Yeye ndiye anayemkataza mwindaji kumpiga mshale Pambo maana kufanya hivyo kungeongeza matatizo badala ya kuyatatua. Kama mzazi ye yote hachoki wala hakati tamaa kumtafuta mwanawe. Tunamwona anavyomgomba Sikitu kwa kutokuwa na huruma na kakaake.

Baba Pambo, kama Wema, ana imani juu ya uchawi. Maneno ya Sikitu yanamfanya atamke . . ." utadhania yeye ndiye kamloga kaka yake (uk. wa 28) Sikitu anaitwa mjinga na wazee wanashauriana la kufanya. Baba Pambo anapendekeza mganga; wazee wenziwe wanamwunga mkono.

"Eheeee! Wewe umesema kweli." (uk. wa 30).

Baada ya kuafikiana hilo, yeye akaendelea kutoa mapendekezo. Juu ya kupatikana kwa mganga, Baba Pambo anamwuliza mwindaji kama kuna kijiji karibu yao. Wanakwenda huku akitamka maneno ya faraja na ya kutia nguvu.

"Matatizo ni mengi, lakini tusife moyo,
Twendeni." (uk. wa 31).

Kuna usemi usemao "bubu kasema kwa uchungu wa mwanawe", nao akina Baba Pambo, kama wazazi wengine wo wote wamejawa na wasiwasi, hofu na mashaka, wote hawana imani sana na mganga, hasa kwa vile mganga mwenyewe afanyavyo mambo ambayo yanawakanganya. Hata hivyo hekima na busara ya Baba Pambo inadhihirika anapowaambia wenzake.

"Tuweni wavumilivu. Tusiseme maneno mengi
kwa vile tu tumechoka na kwa vile tunakutana

na matatizo. Tazameni tulipofika sasa. Tumeweza kuwarudisha watoto wetu maili nyingi kutoka huko walikokuwa. Na kilichotuwezesha kufanya hivyo ni hizo hizo nyimbo mnazozilaumu . . ." (uk. wa 45).

Na jambo lililo wazi kwamba Baba Pambo ni mzazi na ni mtu mzima anayewakilisha hadhi ya wazazi wa Kiafrika, watu wenye hekima na busara juu ya maisha. Ni mtu tunayemkubali na kumhurumia kwa taabu na wasiwasi alionao juu ya mwanawe Pambo; kijana ambaye kwetu sote ni mwanetu.

***Baba Pesa***

Kama Baba Pambo, naye ni mzazi mwenye huruma na uchungu juu ya mwanawe Pesa. Mawazo makuu yanayojitokeza kutokana naye ni "uchungu wa mwana aujua mzazi" na pia shauri lake la kuwapata wanaume wengi zaidi wa kuwasaidia kuwakamata akina Pesa. Inaelekea hana imani kwamba watoto wao wanaweza kupatikana kwa njia nyingine isipokuwa ya nguvu. Baadaye anaunga mkono wazo la kumtafuta mganga. Kadiri mchezo unavyoendelea, Baba Pesa anaonekana kuwa na shaka juu ya Mganga. Haamini kama wimbo unaweza kuwarudisha watoto. Huu ni wasiwasi wa kawaida ambao kila mzazi mwenye kupotelewa na mwanawe anao. Hatimaye anatoa fundo la moyoni mwake:

"Wenzangu, huyu mganga anatudanganya. Anataka watoto wetu wapotee moja kwa moja. Nyie mliona wapi mwenye kichaa kuimbiwa wimbo akapona? Na sisi sote tumekuwa kama wenda wazimu vile vile (uk. wa 45).

Hata hivyo, mganga ana nguvu na kwa maarifa yake wazee wote wanakubali kushirikiana naye katika juhudi za kuwaokoa wana wao. Baba Pesa anaonekana kuwa na haraka zaidi ya kuwakamata watoto wake kuliko Baba Pambo. Hali hii ni nzuri lakini ingefaa zaidi kutuliza bongo na kuwa na makini zaidi kuliko kuwa na harara za paka mwizi.

***Baba Raha***

Naye ni mzazi na mara ya kwanza kabisa tunapokutana naye tunamsikia akimhoji Sikitu juu ya roho yake mbaya (uk. wa 27). Ama yeye ndiye mtu anayeonekana kumfunda Sikitu juu ya utu bora; pia kusema maneno kwa niaba ya wenziwe. Naye kama Baba Pesa ana wasiwasi kuhusu Mganga lakini baadaye anafuata maagizo ya Mganga na wanafanikiwa kuwapata watoto wao.

***Sikitu***

Mvulana mdogo; nduguye Pambo. Ingawa wazazi wa akina Pesa walimwelewa vibaya Sikitu kutokana na maneno yake ambayo kwao yalionyesha kutokuwa na uchungu juu ya hali ya akina Pambo lakini mwenyewe alikuwa na sababu:

"Kwanza huyo kaka mwenyewe mimi sina faida naye.

Tangu kaanza kazi hata senti yake tano siijui. Wala yeye hajui kama ana ndugu yake anayeitwa Sikitu. Sasa vipi mimi nipate taabu kwa sababu yake. Kwa nini mimi nitembee maili na maili, nipigwe na jua, nishikwe na kiu, nivimbe miguu kwa sababu ya mtu asiyenijali? Mwacheni na raha zake za kiwendawazimu, na sisi turudi kwenye raha zetu za kimaskini." (uk. wa 29).

Sikitu ndiye mhusika pekee anayeieleza hali na tabia ya kakaake Pambo na ndiye pia anayesema kweli kwamba wendawazimu wake umetokana na tamaa ya raha za kipuuzi. Kwa maneno mengine Pambo kajitakia hicho kichaa alichonacho. Labda ni kweli kajitakia kwa kutamani mambo asiyo na uwezo nayo na mengine ambayo hayana manufaa naye. Hata hivyo, ilikuwa ni wajibu wa Sikitu kumsumbukia kakaake Pambo kwa hali aliyokuwa nayo. Pambo ni mtoto kimaisha. Kafanya pupa na papara ambayo imemtia katika hali aliyonayo sasa. Ni juu ya Sikitu, ingawa ni mtoto kiumri, amfundishe kakaake utu na faida zake kwa kumfanyia wema na kumwokoa katika janga la wendawazimu. Labda Pambo ataweza kujiuliza na kujirudi. Je, mwalimu na wanafunzi mna maoni gani juu ya Sikitu?

***Mwindaji***

Kwa macho ya kawaida, tunamwona mwindaji akitaka kumpiga mshale Pambo ili kumpunguza nguvu za kichaa chake na kurahisisha kushikwa kwake na kwa wengine pia. Kwa nini anazuiwa kufanya hivyo?

Kwa macho ya moyoni, kumpiga mshale Pambo kuna maana ya kupiga mshale Pambo na tamaa zote ziambatanazo na hali hiyo. Ni kuondoa fikra na mawazo ya kuthamini mapambo na raha zisizo na thamani wala manufaa. Labda ni kweli. Je, wewe una maoni gani?

Zaidi ya hayo, mwindaji ndiye anayetoa msaada wa kupatikana kwa mganga ingawa yeye mwenyewe haoni vipi mganga anaweza kuwashika akina Pambo.

***Mganga***

Anaonekana kuwa mtaalam wa Saikolojia (Elimunafsi) na hasa wa Sakayatri (sayansibongo). Badala ya kutumia nguvu kuwashikia akina Pambo, yeye anatumia maarifa ya kuwapumbaza mpaka wahisi kwamba wao na wazima wote ni vichaa. Anafanikiwa kuwarudisha akina Pambo nyumbani kwa maarifa hayo.

Mganga kwa upande mmoja ni mwakilishi wa mwandishi na kwa upande mwingine ni mwakilishi wetu sisi wasomaji wakati akiwa pamoja na kikundi B. Maswali ya msingi yanayoulizwa ni uhakiki wa kutosha juu ya hali na mategemeo ya wasomi na watu wengine wenye uwezo mkubwa wa kiuchumi. Ama ni maswali mazito ambayo yafaa tuyafikirie na kuyajadili. "Mimi ni Pambo, je, nampamba nani? Kisomo nilichonacho, pesa, kalipa nani?" Tukianza na haya mawili, je, ni huduma zitokanazo na mwenye digrii ndizo za

maana kwa taifa ama ni cheti na joho, ambavyo ni Pambo la huyo msomi tu? Je, Pambo ana wajibu wa kujipamba mwenyewe au kuwapamba wananchi wa taifa lake? Je, wazazi na ndugu zake? Na maswali haya ndiyo yaelekeavyo kuwa majibu ya swali letu la pili linalohusu gharama za kisomo. Na kila mwenye moyò wa shukrani sharti aonyeshe kwa kutoa huduma zenye mafao kwa taifa. Vitendo hivi ndivyo vitakavyodhihirisha dhima yake ya kujenga, kulinda na kuendeleza taifa.

Mganga anauliza swali moja ambalo pia nalo ni kubwa. Inakuwaje kwa mtu mwenye digrii kukosa mamia? (uk. wa 48) labda ni moja katika sababu zimpazo kichaa Pambo. Kikundi B kinaendelea kumsaili Pambo na kikundi chake: Mwingereza kuenda, je, ni nani aliyempinga? Je, ujuzi alionao Pambo ni nani aliyempamba? Huo mshahara mnene wa Pambo ni jasho la nani? Je, hizo pesa ziwekwazo Ulaya zinamfaidia nani? Je, huyo ni Baba Pambo? Je, kuna haki ya Pambo kuwa na pesa zote na wengine wafe kwa njaa? Ni haki kupiga simu tu badala ya kufanya kazi za ofisini? Kuna haja ya kuwa na vyumba sita vya kulala kwa mtu mmoja? Ni kweli Pambo anahitaji wasichana wote kwa manufaa yake?

Mwishoni mganga na Pambo wanashirikiana kuuliza maswali mengi mazito Digrii ninayo, vipi mamia kukosa? Mwingereza kwenda, nani aliyempinga? Je, hayo madaraka niliyo nayo kazini kanipa nani? Je, Pambo anapamba nini?

Mwisho wa yote tunaona hali ya matumaini; uso wa ushindi.

> "Watazamaji wanaendelea kuimba. Wanaanza kutoka kwenye jukwaa, kila baba na mtoto wake, Mganga akiwa mbele yao." (uk. wa 56).
>
> "Na hapa ndipo matumaini na jitihada zetu zinapopata uso mpya—uso wa matumaini; uso wa ushindi." (uk. wa 56).

Mganga na kikundi chake ndio watu wanaoijadili hali ya akina Pambo na kujaribu kutoa suluhishi. Ingawa kila baba anatoka na mtoto wake lakini hatuambiwi nini kinatokea baada ya hapo. Labda maneno ya mwisho ya mganga ndiyo yatowayo jawabu la swali letu—je, kichaa kimepona? Je, Pambo keshapata majibu ya maswali yaliyoulizwa? Je, ataacha tamaa? Au keshapata nyumba, gari, redio, wasichana, n.k.? Je, ni kweli ana pesa nyingi hata benki ishindwe kuziweka? Ama hana kabisa?

**Dhamira**

***Kichaa***

Dhamira kuu ni "kichaa . . . kichaa . . . kichaa. Lakini siyo kichaa cha kutumia nguvu kufanya madhara, bali zaidi kichaa cha mawazo." (Kurasa za 15, 34, 36, 46 na 56). Hii ndiyo dhamira inayojitokeza tangu mwanzo hadi mwisho wa mchezo. Je, kuna sababu zo zote zinazomfanya Pambo awe na kichaa cha mawazo? Labda ni kwa sababu ya kiu cha pesa, kiu cha cheo, kiu cha starehe—magari, nyumba kubwa, mapombe, wasichana na kutokufanya

kazi. Je, ni hizi tu? Je, Pambo alikidhi haja zake hizi? Inawezekana kuwa jawabu yetu ni ndiyo lakini kwa nini apate kichaa tena baada ya kupata vitu vyote hivyo? Inaelekea hakuvipata. Na hii labda ndiyo sababu kubwa ya kichaa chake. Mategemeo na matazamio ya Pambo ni kupata kazi ya madaraka; gari la kwendea kazini na kwingineko, nyumba ya kumhifadhi yeye na familia yake na mshahara mzuri wa kumwezesha aishi badala ya kujaribu ama kuigiza kuishi. Wasichana, mapombe na starehe nyingine ni mahitaji ya ziada ambayo katika baadhi ya nchi si ya lazima na hayafai kabisa. Kwa bahati mbaya mfumo wa jamii na hasa mfumo wa kiuchumi hauruhusu kabisa maisha ayatakayo Pambo na wasomi wenziwe. Je, ni wasomi wote ambao wananyimwa nafasi na uwezo wa kujijengea nyumba zao za kuishi? Labda gari ya kumwezesha afanye kazi zake barabara? Mshahara mzuri wa kutosheleza mahitaji ya maisha? Pambo si mpumbavu kiasi hicho. Labda Pambo mtu lakini Pambo msomi ni mtu anayetarajiwa kuwa na fikira nzito juu ya maisha. Lazima kuna jambo ambalo linamkera na kumkatisha tamaa. Labda aendapo kazini, hapewi kazi kwa sababu ya woga na hofu za baadhi ya wakubwa. Ama hupewa kazi kinyume na kisomo chake. Atokapo kazini hana pa kwenda maana hana nyumba wala chumba. Njiani anapitwa na watu wasiojua vituo vya mabasi; anaona mengi. Mshahara wake unamuwezesha kuishi kwa juma la kwanza tu. Hata benki yake yashindwa kumuwekea pesa zake—si kwa sababu ya wingi wa pesa bali hasa sababu ya wingi wa matatizo na bado kuna watu wasio kama yeye. Je, hali hii haiwezi kumpa mtu kichaa? Wewe waonaje?

***Dogi Seksheni***

Kuna aina maalum ya wasichana wa mijini ambao wanajulikana kwa majina mengi ya kupachikwa. Mojawapo ya hayo ni hili la dogi seksheni na jingine mbwa mwitu, n.k. Majina haya yametolewa kukashifu tabia na mwenendo wa wasichana hao ambao aghalabu mavazi yao ni ya kutisha (achilia mbali mitindo inayokuja na kupita). Si kukashifu tu bali kulaani ila ya kujiuza na kwayo kuliuza taifa na kulivunjia hadhi. Mapenzi yao kwa akina Pambo ni ya pesa (uk. wa 19—21) na labda kwa sababu yao, kina Pambo wanajiongezea matatizo na hatimaye kupata kichaa.

Kijidhamira hichi nacho kina uzito wa namna yake na chahitaji majadiliano makali ili kuona vipi "mwenendo mbaya wa wasichana wetu unavyoathiri mwenendo na hadhi ya taifa letu."

***Taabu ya Kusomesha***

Hapana shaka kila mmoja wetu anajua taabu za kumsomesha mtoto hasa kwa siku za nyuma wakati wazazi walipolazimika kutoa ada kubwa kutokana na mapato yao madogo sana. Masikitiko haya tunayapata na Baba Pambo:

> "Huyu Sikitu mtoto wangu kweli, lakini hana akili. Wewe unajua taabu tulizopata kwa Pambo. Kumsomesha mpaka kufika Chuo Kikuu, mimi nasuka majamvi, mama yako anapika vitumbua. Leo unathubutu kusema tuwaacheni waende wanakotaka? Na wewe pia una kichaa." (uk. wa 28).

Mategemeo na matazamio ya wazazi katika kuwalea na kuwakuza wana wao si malipo bali malezi ya wajibu ambao wana wa Kiafrika tunapaswa kuwa nao. Tumezaliwa na kukuzwa na wazazi wetu, nasi tuna wajibu wa kuwatunza kwa kuwahudumia kwa yote wanayohitaji ila tu kama watataka kufanyiwa majambo yasiyo ya kheri. Masikitiko ya Baba Pambo yanawakilisha wazee wote wa aina yake ambao wana watoto kama Pambo na badala ya kutulia na maisha yao, hutamani vitu na mambo yaliyo juu ya uwezo wao na hatimaye huishia kwenye madhara ya kichaa na kujiharibia maisha kabisa.

Kwa hiyo taabu ya kumsomesha mtoto ni kubwa kwa mzazi na kwa taifa na ni wajibu wetu sisi sote tuliosomeshwa kuwahudumia wazazi wetu kadhalika na kulitumikia taifa letu.

***Imani ya Uchawi***

Imani ya uchawi ni sehemu yenye uzito wa aina yake katika maisha—si ya Kiafrika tu bali ya wanadamu wote wa Ulimwengu huu; tofauti labda ni kwamba sisi twauita *uchawi* na wenzetu huuita *uganga, divine, witchcraft,* n.k. Hofu hii twaipata na Mama Doto:

> "Mimi nakwambia, yule msichana bila shaka kamtupia jini. Yule msichana yuko kishetani shetani. Kamloga Pambo. Simpendi yule msichana. Huwa sipendi apite nje ya nyumba yangu. Sijui Pambo anampenda nini. Kamtupia jini tu, lazima." (uk. wa 19).

Na baadaye Baba Pambo naye anasema:

> "Unamsikia anavyosema. Utadhania yeye ndiye kamloga kaka yake." (uk. wa 28).

Katika maisha, mbali ya imani kwamba kila jambo litokealo hutokea kutokana na nguvu za Mwenye Enzi Mungu, bado baadhi yetu tuna imani kwamba baadhi ya mambo husababishwa na vitendo vya binadamu. Moja katika hayo ni uchawi, kwamba mtu anaweza kumfanyia marogo mtu mwingine na kumdhuru. Suala hili lahitaji majadiliano darasani ili tupate mawazo na maoni juu ya kuweko ama kutokuweko kwa uchawi; je, una manufaa yo yote au ni madhara tu?

***Udugu***

Udugu unaweza kuwa na maana tu kwa watu wanaoelewa maana na thamani yake; vinginevyo, hata watu waliozaliwa tumbo moja wanaweza wasiwe ndugu. Mfano mzuri ni huu wa Pambo na mdogo wake. Sikitu katika kujitetea anasema:

> "Kwanza huyo kaka mwenyewe mimi sina faida naye. Tangu kaanza kazi hata senti yake tano siijui. Wala yeye hajui kama ana ndugu yake anayeitwa Sikitu. Sasa vipi mimi nipate taabu kwa sababu yake. Kwa nini mimi nitembee maili na maili, nipigwe na jua, nishikwe na kiu, nivimbe miguu, kwa sababu ya mtu asiyenijali? (uk. wa 29).

Ni dhahiri kwamba hapa udugu hauna thamani; maana umefikia kiwango hata cha kutojuana majina hali Pambo na Sikitu wamezaliwa pamoja.

Labda ni kwa sababu ya malezi mabaya—hasa siku za nyuma, wakati ambapo watoto waliokwenda shule walionekana kana kwamba ni malaika na wazazi wao. Hali hii ilijenga dharau na chuki kati ya watoto wa familia moja na hata wakuapo hali hubakia hiyo hiyo.

Ikiwa udugu wa familia, mlango, ukoo; unaweza kuwa na tofauti hizi, je, udugu wetu wa kitaifa tuufanyeje ili tuuthamini? Je, kiwango tulichofikia cha udugu wetu chafaa kuwa msingi bora? Je, una mawazo gani kuhusu maneno ya Sikitu kuhusu kakaake?

***Uchungu wa Mwana***

Kijidhamira hiki kimetolewa kwa methali ya kawaida: Uchungu wa mwana aujua mzazi. Mbali ya masikitiko ya Sikitu juu ya kakaake, wazazi wa akina Pambo hawaoni vipi wanaweza kuwaacha watoto wao wapotelee porini. Ni ukweli usio kificho kwamba mzazi ana uchungu mkubwa zaidi kuliko mtu ye yote juu ya mwanawe. Kwa kadiri ilivyo, yeye ndiye mzazi na mlezi wa mtoto wake hata kama ni bozi au kichaa. Kwa upande wetu sisi watoto nasi twapaswa kusema kuwa uchungu wa mzazi aujua mwana. Je, wenzangu mwasemaje?

***Uganga***

Katika mchezo mzima tunamwona Mwindaji peke yake akidhihaki rai ya kumtafuta Mganga wa kuwaokoa akina Pambo:

> Hivyo ndiyo mmeamua kutafuta mganga. Ha, ha, ha! Waganga wapo; twendeni mkachague wenyewe. Lakini leo kweli nimekutana na watu wa ajabu. Twendeni, mie yangu macho tu.

Wengine wote wanakubaliana na wanaamini kuwa Mganga atawasaidia ila Sikitu labda ambaye ana sababu zake nyingine.

Yafaa tuuchukulie uganga katika mapana na marefu yake. Uganga una nguvu. Kuanzia uganga maarifa hadi uganga tiba, wote ni uganga wenye nguvu na athari kubwa kwa imani za watu. Mchezo unadhihirisha nguvu hii kwa kumwezesha Mganga kuwamudu akina Pambo na jamii nzima kwa jumla kwa kuwafanya watu wote vichaa. Maarifa yake ya kuwazuga na kuwapumbaza akina Pambo ni maarifa makubwa yanayoambatana na Saikolojia. Pia Sayansibongo. Na hizi ndizo sifa mbili kubwa za uganga kabla ya hatua ya mwisho ya kumtibu mgonjwa. Je, ni kweli kuwa kila uganga ni ganga? Pambanua na thibitisha kwa mifano itokanayo na ujuzi wa maisha ulionao.

***Wakati wa Kazi ni Kazi***

Maneno ya Mganga (uk. wa 32—33) yanathibitisha kijidhamira hiki.

"Jambo lililo mikononi mwetu ni kubwa na

hatuwezi kupoteza wakati kwa kukaa na
kujiburudisha . . ."

Ni dhahiri kwamba Mganga wetu ni mwanamapinduzi na wa hali ya juu kabisa katika fikira na mwenendo wake. Anawahimiza akina Baba Pambo kuendelea na kazi yao kwa kuwatolea mfano wa maji ya bahari; mfano ambao ni picha nzuri ya hali ya mambo yalivyo maishani. Anasema jinsi maji hayo yasivyoweza kunyweka, wala kuogwa ndivyo watoto wao watakavyokuwa hawafai kwa hili wala kwa lile—iwapo hawatawahi kuwaokoa. Kuharibika kwa Pambo kutakuwa na maana ya kuharibika kwa wasomi wote wa aina yake; na akina Pesa pia, si wao tu bali na wenzao pia. Je, taifa litapata hasara kubwa kiasi gani? Je, tuko tayari kama taifa kuipata hasara hiyo?

Wakati wa kazi ni wa kazi—wakati wa kusoma ni wa kusoma—vinginevyo tutakuwa tukijidanganya wenyewe na kuthibitisha upumbavu tulionao. Je, ni kweli? Wewe una mawazo gani kuhusu umuhimu wa kazi katika ujenzi; ulinzi na maendeleo ya taifa letu?

***Matumizi ya Pesa***

Katika maisha, kila mtu ana mapato yake. Mapato hayo ndiyo yampayo riziki na hifadhi ya maisha yake. Mwingine hupata mapato madogo na mwingine makubwa. Jambo la maana ni kujua namna ya kuyatumia mapato hayo.

Tukitumia mfano wa jamii ya Pambo. Walio wengi wamo katika kiwango cha shilingi elfu moja hadi mbili kabla ya makato ya kodi na michango. Kwa kweli ni wazi kwamba baada ya makato hayo, pesa zitakuwa zimepungua kwa mamia mengi. Pambo amepanga chumba au vyumba labda. Nyumba inadai taa na maji. Akishavilipa hivyo atakuwa amebakiwa na shilingi mia nane au tano labda. Pesa hizi ndizo zilizosalia. Wazazi hawajapewa senti; watoto wa shule, nguo n.k. Na bado Pambo anataka aonekane kuwa ana hela nyingi; mkubwa, Mkurugenzi Meneja. Anataka gari, wasichana wote na jumba la fahari. Je, mtu kama huyu atakosa kuwa na kichaa? Labda analaumu kwamba mshahara ahaopewa ni mdogo; je, taifa lake lina pesa nyingi? Je, jamii yake ina mapato makubwa? Labda anaumizwa na hali za wakubwa ambao ingawa wana jina la mshahara mdogo lakini wana majumba makubwa na mazuri, wana magari ya kuwapeleka kokote watakako kwa haraka na wana misaada ya namna kwa namna. Na labda baadhi ya wakubwa hao ni watu waliosoma pamoja na Pambo. Kwa hiyo Pambo haielewi hiyo hali na hizo tofauti.

Labda masikitiko haya ndiyo yampayo kichaa. Je, wewe unakubaliana naye kwa hayo? Je, na yeye Pambo yuko tayari kumwona kila mwananchi kufikia hali yake? Hili ni tatizo la usawa ambalo kila mtu ana tafsiri nalo mbali na ya mwingine.

Suala letu la matumizi bora ya mapato yetu linatokana na kujijua nafasi

na uwezo wetu maishani. Tusiige na kutamani vitu na hali tusiyo na uwezo nayo. Wewe unaonaje?

***Mvumilivu hula Mbivu***

Hii ni methali ambayo wengi wetu twaijua sana. Kazi yake ni kutupa moyo wa uvumilivu katika mambo yetu tunayoyafanya. Kwa sisi tulioko mashuleni hivi sasa, hapana shaka twajua wajibu wetu na kwamba kufanikiwa kwetu kwategemea sana utii, juhudi na uvumilivu wa hali ya juu. Kadhalika na walimu pamoja na wafanyakazi na wakulima wote.

Kijidhamira hiki kinatolewa na mganga anapowahoji akina Baba Pesa kuhusu harara yao.

> "Basi hamna budi kushirikiana nasi, tusaidiane,
> Muwe wavumilivu na mtakula mbivu." (uk. wa 41).

Kila jambo la maana na la kheri ni gumu na chungu na yahitajika sana kuwa wavumilivu ili tuweze kufanikiwa na haja zetu. Na ni sifa ya utu uzima, hekima na busara.

Katika Pambo, watu wote wamekubali kuigiza mambo ya kichaa mradi wawaokoe watoto ambao ni watoto wa jamii nzima pia. Mganga anawahimiza kwa maneno mazuri yenye hekima kubwa. Anawaambia; "Kulegea kwetu ndiyo kushindwa kwetu" na kwamba kuwaokoa wao ni kuokoa jamii nzima. (uk. wa 46). Kwa nini unadhani kikundi cha akina Pambo kinawakilisha jamii nzima? Una maoni gani kuhusu ari, uvumilivu na juhudi ya mganga?

*Umoja*

Kijidhamira cha mwisho katika mlolongo huu ni hiki kihusucho umoja na ushirikiano. Ni kutokana na moyo mzuri wa upendo na ushirikiano kwamba wazazi na kina Pambo wameweza kupata msaada wa mganga na wa jamii nzima. Moyo huu ndiyo moyo wa kijamaa na kila mmoja wetu anapaswa kujitoa kushirikiana na wenziwe katika mambo na kazi zenye kujenga na kuendeleza taifa letu. Kwa hakika, umoja ni suala zito ambalo lahitaji uongozi bora na kuthaminiana kwa watu wote wa jamii moja ama zaidi. Labda mwalimu atawapa kazi wanafunzi ya kuandika insha au kufanya kongamano au mjadala juu ya umoja, ushirikiano na thamani yake kitaifa.

Ama makala haya yamependekeza dhamira na vijidhamira vya *Pambo.* Ni juu ya mwalimu na wanafunzi kufanya utafiti zaidi ili wapate dhamira na vijidhamira vingi zaidi ya hivi. Pia na kuyatafakari mawazo na maoni yaliyotolewa katika sura hii. Huu ni wajibu wetu walimu na wanafunzi.